

MKATABA WA KUPANGISHA SEHEMU YA BIASHARA

MKATABA HUU umefanyika leo tarehe 26 / 07 / 2024

BAINA YA

JUMA ALLY MUSSA Wa S.L.P 121 Mtaa wa CHAMAKWEZA, Kata ya CHALINZE, Wilaya BAGAMOYO Mkoa wa PWANI, (ambaye katika mkataba huu atajulikana kama “**MWENYE JENGO**”) kwa upande mmoja,

NA

TANZANIA ANSHUN MINING NEW DEVELOPMENT COMPANY LIMITED
PWANI, (ambaye katika mkataba huu atajulikana kama “**Mpangaji**” kwa upande mwingine.

KWA KUWA: -

- a) Mwenye jengo ni mmiliki halali wa Jengo la biashara lililojengwa katika Mkoa wa pwani, wilaya ya bagamoyo.
- b) Mwenye jengo anayo nia ya kupangisha **CHUMBA CHA OFISI** jengo hilo,mpangaji anayo nia ya kupanga sehemu tajwa hapo juu kwa makubaliano yafuatayo.

MKATABA HUU unashuhudia yafuatayo: -

1. Kwamba mwenye jengo atampangisha mpangaji sehemu tajwa hapo juu kwa kodi ya shilingi 1,000,000(milliom moja) Kwa miaka miwili kuanzia tarehe 26/07/2024 hadi tarehe 26/07/2026.
2. Kwamba mpangaji wakati wa kusaini mkataba huu atamlipa mwenye jengo kodi ya miaka miwili (02) ambayo ni sawa na shilingi 2,000,000 (million mbili).

MPANGAJI ANAAHIDI na kuthibitisha kama ifuatavyo: -

3. Kwamba atatumia sehemu hiyo Kwa shughuli za kibiashara tu.
4. Kwamba hatafanya mabadiliko ya kudumu kwenye sehemu hiyo bila kibali cha maandishi toka Kwa mwenye jengo.

5. Kwamba atatunza na kuweka sawa hiyo sehemu ya biashara katika hali ya usafiwakati wotewakati wote, na atalipia gharama za kuondoa uchafu, umeme, maji, ulinzi, na leseni ya biashara yake.
6. Kwamba hatampangisha au kumwachia mtu mwingine sehemu hiyo ya biashara bila idhini ya maandishi toka kwa mwenye jengo.
7. Kwamba atamruhusu mwenye jengo kuingia na kukagua sehemu hiyo kwa madhumuni ya kuifanyia marekebisho ili mradi tu apewe taarifa mapema.
8. Kwamba mwisho wa mkataba atarudisha sehemu hiyo aliyopanga ikiwa katika hali nzuri kama vile yeye alivyokabidhiwa.

MWENYE JENGO nae anaahidi kama ifuatavyo: -

9. Kwamba hatamsumbua wala kumbughudhi mpangaji ilimradi tu mpangaji afuate masharti ya mkataba huu.
10. Kwamba ataendelea kulipia kodi ya kiwanja, jengo na kodi nyingine kama zitakavyotozwa na mamlaka husika.
11. Kwamba atahusika na matengenezo yote yatakayotakiwa kwenye jengo hilo kwa gharama zake mwenyewe.

MKATABA HUU VILEVILE UNASHUHUDIA: -

12. Kwamba iwapo mpangaji atataka kuendelea kupanga sehemu tajwa atalazimika kutoa taarifa ya mwezi mmoja kabla ya muda kuisha na akikubaliwa kupanga ataendelea kupanga kama watakavyokubaliana na mwenye jengo.
13. Mkataba huu utalindwa, kutafsiriwa na kusimamiwa na sheria za ardhi na mikataba za Tanzania.
14. Mkataba huu utanza mara tu baada ya kusainiwa na pande zote mbili zinazohusika.

KWA KUTHIBITISHA makubaliano hayo pande zote mbili zimetia saini zao kama ifuatavyo;

UMETIWA SAINI na KUPOKELEWA

JUMA ALLY MUSSA aliyetambulishwa kwangu na ambaye ninamfahamu hapa PWANI

[Handwritten Signature]
.....

MWENYE JENGO

leo tarehe ²⁶.....mwezi ⁰⁷.....2024.

witness to the above signature:

Name: SAID MEHD SELEDANI

Signature: *[Handwritten Signature]*

Postal Address: P.O. Box 3444, DSM

Qualification: ADVOCATE



UMETIWA SAINI na KUPOKELEWA na

TANZANIA ANSHUN MINING NEW DEVELOPMENT hapa mkoa wa pwani

leo hii tarehe ²⁶..... mwezi ⁰⁷2024

[Handwritten Signature]
.....

MPANGAJI

MBELE YANGU

witness to the above signature:

Name: SAID MEHD SELEDANI

Signature: *[Handwritten Signature]*

Postal Address: P.O. Box 3444, DSM

Qualification: ADVOCATE

